



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA BUKOBA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa)

MUHTASARI: 04/2021-2022

**KIZIDO CHA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE
23.11.2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA**

MAHUDHURIO:

1. Dr. Mustafa Waziri	Mwenyekiti
2. Severian Buhaga	Katibu
3. Francis L. Nshaija	Mjumbe
4. Dotto Tambuko	Mjumbe
5. Catres Rwegasira	Mjumbe
6. Adv. Athuman Msosole	Mwanasheria

WASIOHUDHURIA:

1. Dr. Alphonse Bagambabyaki - Mjumbe - kwa taarifa

WAALIKWA;

- | | |
|---------------------|--|
| 1. Debora Ngangaji | - Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |
| 2. Method Rwelamila | - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |

SEKRETARIETI:

1. Arafa King
2. Jospide Majaba
3. Edina Bingola
4. Maria Joseph

AGENDA ZA KIKAO:

Ajenda za kikao zilithibitishwa na Wajumbe kama ifuatavyo :-

- 1.Kufungua kikao
- 2.Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa tarehe 10/11/2021
- 3.Kupitia taarifa ya Mkurugenzi kuhusu Zabuni ya kufunga taa 227 za mionzi jua kwenye Barabara 4 zenye urefu wa kilometa 8.8 katika Manispaa ya Bukoba
4. Kupokea taarifa ya Mkurugenzi kuhusu Zabuni ya ununuzi wa mashine ya kufyatua matofali
- 5.Kupitia taarifa ya Mkurugenzi kuhusu Zabuni ya pikipiki kwa ajili watendaji wa kata na idara ya fedha.
- 6.Ombi la kutumia Force Account kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa vyumba vya Madarasa 30 , Utengenezaji wa Viti 1500 na Meza 1500 kupitia mradi wa TCRP 5441 2021
- 7.Kufunga kikao.

MUHT.NA. 01/04/2021/22 - KUFUNGUA KIKAO:

Katibu aliwakaribisha wajumbe ukumbini na kutoa taarifa kuwa Mwenyekiti wa Bodi amesafiri .Hivyo kwa mujibu wa taratibu za vikao aliwaomba wajumbe wamuchague Mwenyekiti wa kikao . Baada ya kusema hayo aliwakaribisha wajumbe kwa ajili ya kuchagua Mwenyekiti.Wajumbe kwa pamoja walimchagua Dr.Mustafa Waziri kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kumuchagua na kuwaomba Wajumbe kuchangia ajenda zilizoandaliwa ili maamuzi yatakatayofikiwa yawe ya kuleta tija katika Halmashauri ya Manispaa Bukoba. Baada ya kusema hayo alifungua kikao 3.20 Asubuhi.

MUHT.NA. 02/04/2021/22 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 10/11/2021.


Muhtasari ulisomwa kwa sauti mbele ya Wajumbe kisha ukathibitishwa na Katibu na Mwenyekiti kama kumbukumbu sahihi za kikao .

MUHT.NA.05/04/2021/22 –OMBI LA KUTUMIA FORCE ACCOUNT KWA AJILI YA UTEKELEZAJI UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 30, UTENGENEZAJI WA VITI 1500 NA MEZA 1500 KUPITIA MRADI WA TCRP 5441 2021

Ombi la kutumia **Force Account** wakati wa utekelezaji wa fedha za mradi wa **TCRP 5441 2021** liliwasilishwa , ilielezwa kuwa kiasi cha Tshs 600,000,000.00 kimetumwa moja kwa moja katika shule 14 za Sekondari kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya Madarasa 30, viti 1500 kama kiambata kinavyoonesha. Taarifa iliwasilishwa na kujadiliwa kisha wajumbe kwa pamoja walikubaliana utekelezaji wa mradi huu utekelezwe kwa njia ya **Force Account** . Aidha, ilisisitizwa kuwa utekelezaji wa mradi huu unatakiwa ukamilike kabla au ifikapo tarehe 15.12.2021 .

MUHT.NA. 06/04/2021/22 –KUFUNGA KIKAO.

Katibu alimshukuru Mwenyekiti kwa jinsi alivyoendesha kikao pia aliwashukuru Wajumbe kwa jinsi walivyochangia ajenda zilizokuwa zimeandaliwa. Baada ya kusema hayo alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao. Mwenyekiti alifunga kikao saa 12.00 Mchana kwa kuwashuru Wajumbe jinsi walivyochangia ajenda zilizokuwa zimeandaliwa na aliwatakia kazi njema.



Mwenyekiti

UMETHIBITISHWA



Katibu

Tarehe 30/11/2021

**UJENZI WA VYUMBA 30 KWA SHULE ZA SEKONDARI KWA
FEDHA MRADI WA TCRP**

S/N	HALMASHAURI	JINA LA SHULESHULE	IDADI YA MADARASA	FEDHA POKELEWA	IDADI YA VITI NA MEZA	
					KITI	MEZA
1	BUKOBA MC	BAKOBA	2	40,000,000.00	100	100
2	BUKOBA MC	BILELE	2	40,000,000.00	100	100
3	BUKOBA MC	BUHEMBE	2	40,000,000.00	100	100
4	BUKOBA MC	HAMUGEMBE	2	40,000,000.00	100	100
5	BUKOBA MC	IJUGANYONDO	2	40,000,000.00	100	100
6	BUKOBA MC	KAGEMU	1	20,000,000.00	100	100
7	BUKOBA MC	KASHAI	3	60,000,000.00	100	100
8	BUKOBA MC	KIBETA	2	40,000,000.00	50	50
9	BUKOBA MC	NSHAMBYA	3	60,000,000.00	100	100
10	BUKOBA MC	NYANGA	2	40,000,000.00	150	150
11	BUKOBA MC	RUMULI	3	60,000,000.00	100	100
12	BUKOBA MC	RUTUNGA	2	40,000,000.00	100	100
13	BUKOBA MC	RWAMISHENYE	2	40,000,000.00	150	150
14	BUKOBA MC	RWAZI	2	40,000,000.00	150	150
JUMLA			30	600,000,000.00	1500	1500